BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

# BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Nane – Tarehe 23 Septemba, 2024**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. **TAARIFA YA SPIKA:**

II. **HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kwa mwaka 2023/2024.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kwa mwaka 2023/2024.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kuhusu Ripoti ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo juu ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kwa mwaka 2023/2024.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kuhusu Ripoti ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale juu ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kwa mwaka 2023/2024.

## III. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

37. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Kwa kuwa mapambano ya changamoto ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi ni masuala ya kikanda na kimataifa.

Kwa kiasi gani Serikali ya Zanzibar imeyafikia mashirika ya kikanda na kimataifa katika mapambano haya.

### Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

264. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Makaburi ya Mwanakwerekwe ni eneo muhimu ambalo jamii kubwa ya wananchi hulitegemea kwa huduma ya mazishi. Licha ya huduma muhimu zinazotolewa katika eneo hilo kwa kuwahifadhi wenzetu waliotangulia mbele ya haki, kuna tatizo la kusahaulika kwa eneo hilo na kupelekea vitendo visivyo vya heshima kufanyikia hapo.

(a) Je, kwa kiasi gani Serikali inaifahamu changamoto hii inayoikabili eneo hili ikiwa ni pamoja na kukosa uzio, hali inayopelekea vitendo viovu kufanyika katika maeneo hayo.

(b) Je, Serikali inachukua hatua zipi kulilinda eneo hili muhimu ambalo lina maana kubwa kwa imani zetu za kidini.

(c) Ni mipango ipi iliyowekwa na Serikali ya kuyatenga na kuyalinda maeneo kama haya kwa ajili ya makaburi, ili kuhakikisha kuwa yanatunzwa kwa heshima na usalama wa hali ya juu.

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu:**

31. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu:

    Tunaipongeza Serikali kwa kuanzisha mifumo mbali mbali ya TEHAMA kwa ajili ya kurahisisha huduma inazozitoa.

    Ni kwa namna gani mifumo hiyo imeongeza uwajibikaji kwa watumishi wa umma.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

55. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

    Ni lini Serikali itawekeza kimkakati kwenye tasnia ya tafiti mbali mbali zitakazoleta mageuzi makubwa ya kiuchumi.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

11. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

    Natambua juhudi za Serikali katika kuiwezesha Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) kufunguwa matawi mbali mbali nje ya Zanzibar.

    Ni lini benki hii itakuwa na tawi angalau moja kwa kila Mkoa huko Tanzania Bara.

12. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

    Kumekuwa na malalamiko kuwa mifumo ya ukusanyaji wa fedha haisomani na kupelekea upotevu wa fedha za umma.

    Ni lini Serikali itakamilisha suala la kuunganisha mifumo yake, ili kuokoa fedha za umma na kuongeza ufanisi Serikalini.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

38. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Asilimia kubwa ya Serikali za Mitaa hazifikii malengo ya ukusanyaji wa mapato iliyojipangia.

Je, Serikali Kuu imefanya tathimini ili kujua ni sababu zipi zinazopelekea Serikali za Mitaa kutofikia malengo yake hayo.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

59. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Ni aina gani ya maradhi ambayo kwa pamoja yanawapata binadamu na wanyama kwa wakati mmoja.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

3. MHESHIMWA MWANAJUMA KASSIM MAKAME (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar:

Kwa nia njema Serikali yetu iliamua kuanzisha elimu mjumuisho mashuleni, ambayo pamoja na juhudi hizo za Serikali, inakabiliwa na changamoto mbali mbali ikiwa ni pamoja na upungufu wa vifaa vya kufundishia na uhaba wa walimu kwa wanafunzi. Changamoto hizo zinarudisha nyuma kasi na azma njema ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

(a) Ni hatua zipi ambazo Serikali imelenga kuzichukua katika kutatua changamoto hizo.

(b) Sababu gani zinazopelekea upungufu wa vifaa vya kufundishia, mashine za kujifunzia na walimu kwa wanafunzi wa elimu mjumuisho nchini.

**<u>Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:</u>**

228. MHESHIMIWA JUMA ALI KHATIB (Uteuzi wa Rais) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Serikali imechukua juhudi za kukifanyia matengenezo Kiwanja cha Kimataifa cha ‘New Aman Complex’ kwa lengo la kuziwezesha timu za ndani na nje ya Zanzibar kuutumia katika mashindano tofauti. Hivi karibuni timu zetu za Jeshi la Kujenga Uchumi na timu ya Uhamiaji zilifanikiwa kuiwakilisha Zanzibar katika mashindano ya CAF ambazo kiutaratibu mashindano hayo huchezwa kwa awamu mbili (ndani ya nchi husika ‘home ground’ na marudiano ‘away’).

(a) Kwa nini timu zetu zinazoshiriki mashindano hayo zimekosa uzalendo kwa kuamua kucheza mechi zao zote nje ya Zanzibar.

(b) Je, kwa vile Zanzibar ni nchi salama na inao uwanja wenye hadhi ya kuchezwa mechi za kimataifa, kwa nini timu hizo zimevunja masharti ya FIFA yanayotaka mechi hizo kuchezwa sehemu mbili.

(c) Je, Serikali haioni kuziwachia timu hizo kucheza mechi zao katika nchi za ugenini ni kuwakosesha wananchi wazalendo kupata burudani na kudumaza vipaji vya ndani.

242. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Pamoja na jitihada za kujikwamua kimichezo, moja ya changamoto inayolikabili soka la Zanzibar ni uwepo wa Tanzania Football Federation (TFF) ambayo ndiyo taasisi inayotambuliwa na mashirika ya kimataifa kama vile FIFA na CAF.

(a) Ni mfumo gani unaotumika wa mgawanyo wa misaada na fedha zinazopitia TFF kwa Zanzibar, na ni vigezo vipi vinatumika katika ugawaji huu.

(b) Serikali inaisaidia vipi Zanzibar kupata faida ambazo TFF inazipata katika kuendeleza soka.

(c) Je, Serikali ina mipango gani ya kuhakikisha kwamba Zanzibar inashirikishwa kikamilifu katika mchakato wa maamuzi ya kitaifa na kimataifa yanayohusiana na michezo.

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:**

159. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Hivi karibuni tumemshuhudia Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi akizindua bustani miongoni mwa bustani bora kabisa ya Mnazi Mmoja.

Ni lini Serikali itajenga aina ya bustani kama hizi kwa ajili ya wazee tu, ili wapate sehemu ya kupunguza misongo ya mawazo, kama zinavyojengwa bustani kama hizo katika nchi nyengine zilizopiga hatua ya kimaendeleo duniani.

**Wizara ya Afya:**

10. MHESHIMIWA AZZA JANUAR JOSEPH (Nafas iza Wanawake) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa kuwa wananchi wengi wanaosumbuliwa na maradhi ya UKIMWI pamoja na kifua kikuu wanapaswa kutumia dawa kwa muda mrefu, na kwa kuwa uelewa mdogo kwa wagonjwa hao hupelekea matumizi ya dawa hizo kuzikatiza bila ya ruhusa ya daktari, jambo linalowaletea usugu wa maradhi yao.

(a) Ni kwa kiasi gani Wizara yako inalitambua suala hili.

(b) Ni hatua gani muhimu ambazo Wizara yako inazichukuwa katika kulitatua tatizo hili.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

205. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Ni lini Serikali itajenga kiwanda cha kuchakata matunda ili kudhibiti na kufanya matumizi mbadala wa matunda yanayozagaa kutokana na ujenzi wa masoko mapya makubwa na ya kisasa nchini.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

### Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kwa mwaka 2023/2024.

### Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kwa mwaka 2023/2024.

### Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati Utalii, Biashara na Kilimo kwa mwaka 2023/2024.

**Zanzibar,**
**23 Septemba, 2024.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**